

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Singida*  
16 Oktoba, 2023

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS SAMIA AWATAKA WANANCHI KUJIELEKEZA KWENYE FURSA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewataka viongozi mkoani Singida kuwa na mikakati ya kutumia fursa za kiuchumi badala ya kujikita kwenye sekta moja tu ili kuongeza kasi ya maendeleo ya mkoa huo.

Rais Samia ametoa tamko hilo leo wakati akihutubia wananchi katika maadhimisho ya miaka 60 ya mkoa huo yaliyofanyika katika uwanja wa *Bombadia*.

Aidha, Rais Samia amewataka viongozi kuwahamasisha wananchi kupanda mazao yanayostahamili ukame pamoja na kutumia mbegu bora na za muda mfupi.

Rais Samia pia amewahimiza wananchi kulima mazao ya alizeti, dengi na ufuta ambayo hustawi katika maeneo mengi ya mkoa wa Singida pamoja na zao la korosho ambalo pia linafanya vizuri katika maeneo mengi ya mkoa huo.

Vile vile, Rais Samia ameiagiza Wizara ya Kilimo kuhakikisha miradi ya umwagiliaji inatekelezwa katika maeneo yote yaliyobainishwa kwa ajili ya ujenzi wa skimu.

Awali Rais Samia alizindua daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 lililopo Wilaya ya Mkalama ambalo limegharimu kiasi cha takribani shilingi bilioni 11.2.

Akihutubia wananchi wa Mkalama Rais Samia amesema Serikali itaendelea kushughulikia changamoto za kissekta zinazoikabili wilaya hiyo hususan elimu, afya na maji.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

